




HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU
MTIHANI WA MUHULA WA PILI DARASA LA TATU
SHULE YA MSINGI NAMPUNGU



SOMO: SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MUDA: SAA 1:30

Novemba,

2026

JINA LA MWANAFUNZI:

1. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano

i. Utabiri wa matokeo ya kubuni kuhusu tatizo fulani huitwaje?

A. jaribio B. hitimisho C. Dhanio D. tatizo ()

ii. Binadamu ana milango ya fahamu mitano. Je, ni mlango upi wa fahamu huhusika na kuhisi hali mbalimbali kama vile joto, baridi na mguso?

A. macho B. masikio C. ulimi D. Ngozi ()

iii. Ni Kundi lipi la viumbe ambao huzaa Watoto na kunyonyesha?

A. amfibia B. reptilia C. ndege D. mamalia ()

iv. Kuna mimea inayozaliana kwa kutoa maua na isiyotoa maua. Je, ni mmea upi kati ya ifuatayo hautoi maua?

A. maharage B. mahindi C. kunde D. mvinje ()

v. Teknolojia ya habari na mawasiliano hutuwezesha kupata habari na elimu mbalimbali. Je, ni kifaa kipi kati ya vifuatavyo si kifaa cha TEHAMA?

A. simu B. gari C. redio D. kompyuta ()

2. Oanisha maelezo kutoka kifungu A na hatua kutoka kifungu B.

KIFUNGU A	MAJIBU	KIFUNGU B
i. Hatua ya kwanza ya uchunguzi wa kisayansi	()	A. Kuchambua data
ii. Utabiri wa matokeo ya jaribio la kisayansi	()	B. Hitimisho
iii. Kuzipanga data, kuzichambua na kuziweka katika utaratibu mzuri	()	C. Kubaini tatizo
iv. Hatua ambayo huthibitisha au kukanusha dhanio	()	D. Kuandika taarifa
v. Hatua ya mwisho ya uchunguzi wa kisayansi	()	E. Dhania

3. Chagua kundi la wanyama katika sanduku kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

amfibia

reptilia

samaki

mamalia

ndege

- i. Binadamu, ng'ombe, mbuzi na popo ni wanyama katika kundi la
- ii. Kenge, mamba, mjiusi na kobe ni baadhi ya wanyama katika kundi la
- iii. Chura ni wanyama katika kundi la
- iv. Kuku, kanga na tausi ni wanyama katika kundi la
- v. Perege na Kambale ni wanyama katika kundi la

4. Soma habari kisha jibu maswali yanayofuata.

Sayansi ni maarifa yanayopatikana kwa kufanya uchunguzi na majaribio. Uchunguzi na majaribio hufanyika ili kubaini ukweli wa mambo. Sayansi ina matawi makuu matatu ambapo kila tawi linahusika na aina fulani ya maarifa. Matawi hayo ni Fizikia na Kemia na Baiolojia. Fizikia ni tawi la sayansi linalohusu uhusiano wa maada na nishati, Kemia ni tawi la sayansi linalohusu muundo na tabia za maada na mabadiliko yanayotokea katika maada na Baiolojia ni tawi la sayansi linalohusu viumbehai.

Maswali

- i. Kwanini tunafanya uchunguzi na majaribio ya kisayansi?
- ii. Ni tawi lipi la sayansi linalohusu uhusiano wa maada na nishati?
- iii. Ni tawi lipi la sayansi linalohusu muundo, tabia na mabadiliko ya maada?
- iv. Maarifa yanayopatikana kwa kufanya uchunguzi na majaribio yanaitwaje?
- v. Fabian anataka kuwa daktari wa binadamu. Je, ni tawi gani la Sayansi itabidi kulisomea zaidi?


5. Chunguza picha hapo chini kisha jibu maswali yafuatayo.



1



2



3

- i. Taja jina la ogani iliyoonyeshwa kwa namba 1
- ii. Taja jina la ogani iliyoonyeshwa kwa namba 2
- iii. Taja jina la ogani iliyoonyeshwa kwa namba 3
- iv. Taja kazi ya ogani iliyoonyeshwa kwa namba 1
- v. Taja kazi ya ogani iliyoonyeshwa kwa namba 2